

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 022 2112065-7  
Fax No. +255 022 2112538  
E-mail: [info@bunge.go.tz](mailto:info@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 9133,  
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MASHINDANO YA MABUNGE YA AFRIKA  
MASHARIKI (INTER-PARLIAMENTARY GAMES) YATAKAYOFANYIKA JIJINI DAR ES  
SALAAM TAREHE 1 HADI 11, DESEMBA, 2017.**

Kama ambavyo Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Ndugai, aliwatangazia waheshimiwa Wabunge na Umma kwa ujumla siku ya tarehe 17/11/2017 wakati wa kuahirisha Mkutano wa Tisa wa Bunge uliomalizika hivi karibuni Mjini Dodoma, mwaka huu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni wenyeji wa mashindano ya michezo mbalimbali inayochezwa na timu za Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi hizo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan ya Kusini. Aidha, timu ya Bunge la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) nayo ni miongoni mwa timu zitakazoshiriki katika mashindano haya.

Mashindano haya yatakatayofanyika kwenye viwanja vya Taifa jijini Dar es Salaam kuanzia Desemba 1 hadi 11, 2017 yatahusu michezo ya soka, pete, wavu kwa wanaume, wavu kwa wanawake, gofu kwa wanawake, gofu kwa wanaume, kuvuta kamba wanawake, kuvuta kamba wanaume, riadha kwa wanawake, riadha kwa wanaume, na kutembea kwa mwendo kasi kwa wanaume na wanawake. Mashindano ya michezo hii ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Treaty).

Pamoja na kwamba mashindano haya yatarushwa mubashara (Live) na baadhi ya vituo vya Radio na Televisheni, timu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Bunge Sports Club) inawaalika watanzania na wananchi kwa ujumla, hususan wakazi wa jiji la Dar es Salaam na mikoa ya jirani, kuhudhuria mashindano hayo ili kushuhudia vipaji vya michezo walivyo navyo waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa taasisi za Bunge.

Kwa sasa timu ya Bunge la Tanzania imejichimbia jijini Dar es Salaam ikiendelea na mazoezi kabambe kwa lengo la kuibuka bingwa katika michezo yote.

Ushiriki wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utakaongozwa na Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai, pia utahusisha waheshimiwa Wabunge na viongozi mbali mbali wa kitaifa.

Aidha, Timu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawashukuru kwa dhafi wadhamini mbali mbali waliojitokeza kuwezesha ushiriki wa timu yetu katika mashindano haya. Tunakusudia kutoa taarifa rasmi kuhusu wadhamini wetu siku chache zijazo.

Bunge Sports Club - Tanzania inavishukuru sana Vyombo vya Habari na Wananchi kwa ujumla kwa kutuunga mkono tangu tulipokuwa kambini mjini Dodoma, hadi sasa tukiwa hapa jijini Dar es Salaam.

Asanteni sana.

**Imetolewa na:-** William M. Ngeleja, Mb,  
Mwenyekiti,  
Bunge Sports Club – Tanzania.

29 Novemba, 2017.